JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



# MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

OKTOBA 2024

**DIBAJI**

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Na.2 ya mwaka 2019 kupitia Tangazo la Serikali GN.459 la tarehe 14 Juni 2019. Taasisi hii ni ya Muungano na ina majukumu ya kutoa huduma za hali ya hewa, kudhibiti, pamoja na kuratibu shughuli za hali ya hewa nchini. Aidha, Mamlaka ina jukumu la kuiwakilisha nchi katika masuala ya hali ya hewa kimataifa.

Mkataba huu umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa Serikali wa kuandaa mikataba ya huduma kwa wateja wa mwaka 2013. Mkataba unaainisha nia ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ya kuboresha utendaji na utoaji huduma bora kwa umma kwa lengo la kuwaridhisha wateja na watumiaji wengine wa huduma za hali ya hewa kulingana na mahitaji na matarajio yao. Kwa vile mkataba huu ni chombo hai, utekelezaji wake utafuatiliwa kwa makini na matokeo yatatumika kuufanyia marekebisho pale inapobidi ili kwenda sambamba na matarajio ya wateja.

Mkataba huu unaainisha aina ya wateja, huduma zitolewazo na viwango vyake, wajibu wa mtoa huduma (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania) na haki na wajibu mteja. Mkataba pia unatoa nafasi kwa mteja kutoa mrejesho, na njia mbalimbali za mawasiliano zimeainishwa ili kumsaidia mteja kuifikia Mamlaka.

Nawasilisha mkataba huu kwa mteja na wadau wa huduma za hali ya hewa nchini ili wafahamu huduma zitolewazo na Mamlaka ikiwemo huduma za kijamii na kibiashara, viwango vya huduma na upatikanaji wake. Aidha, ni matarajio yangu kuwa mtaendelea kutumia huduma zetu na kutoa mrejesho kwa lengo la kuisaidia Mamlaka kuendelea kuboresha huduma zake ili kukidhi au kuzidi matarajio ya mteja.

Nawatakia ushirikiano mwema katika utekelezaji wa mkataba huu.

09/10/2024

Dkt. Ladislaus B. Chang’a
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

## YALIYOMO


*DIBAJI* ..................................................................................................... *ii*

*MAANA YA VIFUPISHO* ..................................................................................... *iv*

*FASIRI YA MANENO* ........................................................................................ *v*

*DIRA, DHIMA NA MAADILI YA MSINGI YA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA* ............................................................................................... *1*

**Dira.** ..................................................................................................... **1**

**Dhima.** ..................................................................................................... **1**

**Maadili.** ..................................................................................................... **1**

*WATEJA WETU* .............................................................................................. *2*

*HUDUMA ZETU* ............................................................................................. *2*

*VIWANGO VYA HUDUMA ZETU* ........................................................................ *3*

*WAJIBU WA MAMLAKA KWA MTEJA* ................................................................ *7*

*HAKI NA WAJIBU WA MTEJA* ........................................................................... *7*

**Haki za mteja** ............................................................................................. **7**

**Wajibu wa mteja** ........................................................................................... **8**

*MREJESHO WA UTOAJI HUDUMA* .................................................................... *8*

*UTAMBULISHO WA MAMLAKA NA NJIA ZA MAWASILIANO;* ................................. *9*

**Ofisi kuu za utabiri** ...................................................................................... **10**

**Vituo Vikuu vya Hali ya Hewa** ........................................................................ **11**

## MAANA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |
| **ICAO** | Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga |
| **ISO** | Shirika la Kimataifa la Viwango |
| **JNIA** | Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere |
| **NACTE** | National Council for Technical Education |
| **PSRP** | Public Sector Reform Program |
| **TAMISEMI** | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TMA** | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania |
| **WMO** | Shirika la Hali ya Hewa Duniani |

## FASIRI YA MANENO

**Mteja:** Taasisi au mtu anayehitaji na kupewa au kununua huduma

**Mamlaka:** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

**Utabiri:** Matarajio ya kisayasi ya hali ya hewa ya muda mfupi na muda wa kati (sasa hadi wiki mbili) ujao

**Mdau:** Taasisi au mtu mwenye maslahi na utendaji wa TMA

**Tsunami:** Mfululizo wa mawimbi makubwa katika bahari au maziwa makubwa yanayosababishwa na kuhamishwa kwa kiasi kikubwa cha maji kutokana na tetemeko la ardhi chini au karibu na sakafu ya bahari.

**DIRA, DHIMA NA MAADILI YA MSINGI YA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

**Dira**

Kuwa kitovu bora cha utoaji huduma za hali ya hewa kwa maendeleo enedelevu ya kiuchumi na kijamii.

**Dhima**

Kuhakikisha uwepo wa huduma bora na za uhakika za hali ya hewa, zinazokidhi matarajio ya wadau kupitia utoaji na udhibiti wa huduma za hali ya hewa kwa usalama na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania.

**Maadili**

Katika kutekeleza dira na dhima ya Mamlaka, tunahakikisha utendaji unaozingatia yafuatayo:

| Na. | Maadili ya msingi | Maelezo |
|---|---|---|
| 1. | **Utaalamu** | Kuzingatia taaluma ya hali ya juu ili kukidhi mahitaji ya umahiri; |
| 2. | **Uwazi na Uwajibikaji** | Tutalazimika kutoa huduma bora za uhakika za hali ya hewa ili kukidhi matarajio ya wateja; |
| 3. | **Ujumuishaji anuwai** | Tutatoa huduma zetu kwa wadau bila ubaguzi wa rangi, kabila, jinsia, ulemavu, utaifa, nafasi zao kijamii na kiuchumi, n.k.; |
| 4. | **Huduma bora na kwa wakati** | Tutatekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia weledi na ubora wa huduma tunazotoa kwa muda muafaka |
| 5. | **Ufanisi** | Tutatumia njia ya gharama fanisi zaidi kutimiza matarajio ya wadau wetu kupitia uboreshaji endelevu utakaohakikisha ukuaji na uthabiti |
| 6. | **Utendaji wa pamoja** | Tunadhamiria kufanya kazi katika mazingira ambayo mchango wa kila mfanyakazi unathaminiwa, unaheshimiwa, unatambuliwa na mfanyakazi huyo anatuzwa kwa juhudi zake |
| 7. | **Mteja kwanza** | Tunamjali mteja kwa kutoa huduma bora zinazokidhi au kuzidi matarajio yake. |

## MADHUMUNI YA MKATABA

Madhumuni ya mkataba huu ni kumwezesha mteja azifahamu huduma zinazotolewa na Mamlaka na viwango vya huduma hizo. Mkataba pia unaelezea wajibu wa Mamlaka katika kutoa huduma bora, haki na wajibu wa mteja katika kupata huduma husika. Vile vile, Mkataba unaainisha namna mteja atakavyotoa mrejesho kuhusiana na huduma inayotolewa.

## WATEJA WETU

Wateja wa mamlaka ya hali ya hewa ni kama ifuatavyo;

i. Wizara/ Idara za kujitegemea/Sekretarieti za Mikoa/Wakala wa Serikali/Mamlaka za Serikali za mitaa/Mashirika ya Umma na Taasisi;
ii. Wadhibiti na vyama vya wadhibiti;
iii. Vyombo vya habari na mawasiliano;
iv. Vikosi vya ulinzi na usalama nchini;
v. Asasi za Kiraia (AZAKI);
vi. Washirika wa maendeleo na taasisi za kimataifa;
vii. Wanataaluma na taasisi za utafiti na elimu;
viii. Watoa huduma;
i. Wanasiasa/Bunge;
ii. Umma.

## HUDUMA ZETU

i. Utabiri wa hali ya hewa
ii. Data za hali ya hewa
iii. Usimikaji na Usajili wa Vituo vya hali ya hewa
iv. Uangazi wa hali ya hewa
v. Mafunzo
vi. Ushauri Elekezi
vii. Andiko na Jarida la kitafiti la Hali ya Hewa
viii. Malipo mbalimbali
ix. Huduma nyinginezo

**VIWANGO VYA HUDUMA ZETU**

Mamlaka ya Hali ya Hewa inaanisha viwango vya huduma zinazotolewa kama ifuatavyo;

1. **Utabiri wa hali ya hewa**

   **i.** Tutatoa utabiri wa hali ya hewa wa **kila siku na siku tano** kwa vyombo vya habari, tovuti na mitandao ya kijamii **kati ya saa 9 hadi saa 11 jioni** kila siku;

   **ii.** Tutatoa utabiri wa hali ya hewa **wa siku kumi na mwezi** kwa vyombo vya habari, tovuti na mitandao ya kijamii na Siku ya mwisho ya kila siku kumi za kila mwezi na kila siku ya mwisho wa mwezi;

   **iii.** Tutatoa Mwelekeo wa hali ya hewa ya misimu kwa vyombo vya habari, tovuti na mitandao ya kijamii kwa kila msimu kama ifuatavyo;

   - Vuli (Septemba/Oktoba hadi Disemba): Mwezi wa Agosti;
   - Msimu (Novemba hadi Aprili): Mwezi wa Oktoba;
   - Masika (Machi hadi Mei): Mwezi wa Februari;
   - Kipupwe (Juni hadi Agosti): Mwezi wa Mei;

   iv. Tutatoa tahadhari za hali mbaya ya hewa (upepo mkali, vimbunga, tufani, upungufu wa mvua, mvua kubwa, joto/baridi kali, majivu ya volcano, hali ya hewa inayoathiri uono (visibility)) zenye kiwango cha usahihi cha 70% au zaidi;

   v. Tutatoa utabiri kwa usafiri wa anga kwa kufuata miongozo ya kitaifa nakimataifa (WMO, ICAO na ISO 9001);

   vi. Tutatoa utabiri wa hali ya hewa kwa shughuli na usafiri baharini na kwenye maziwa kulingana na miongozo ya kitaifa na kimataifa (WMO na IMO);

   vii. Tutatoa utabiri wa hali ya hewa kwa shughuli mahsusi mfano; mafuta na gesi, viwanda, utalii na michezo, Ujenzi, uzalishaji nishati, uchimbaji madini, benki na bima, kilimo, mifugo, rasilimali za maji, usimamizi wa mazingira, usafiri wa ardhini na miundombinu yake na uendeshaji mitandao ya simu za mkononi, kwa kuzingatia makubaliano kati ya mteja na TMA.

2. **Data za hali ya hewa**

   Tutatoa data na ushauri wa kitaalam kwa mteja kwa kuzingatia sera na kanuni za Mamlaka ndani ya siku 3 za kazi baada ya mteja kukamilisha taratibu zote.

**3. Usimikaji na Usajili wa Vituo vya hali ya hewa**

| Huduma | | Viwango |
|---|---|---|
| **a.** | **Usimikaji (installation)** | |
| i. | Kituo kinachojiendesha chenyewe (Automatic Weather Station-AWS) | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| ii. | Kituo kinachoendeshwa na mtu (Manned weather station) | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| iii. | Kituo cha kupima mvua | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| *iv.* | *Rada (*Radar*)* | Siku 30 hadi 60 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| *v.* | *Kituo cha uangazi cha anga la juu (Upper air station)* | Siku 30 hadi 60 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| *vi.* | *Vifaa vya utambuzi vya matukio ya radi (Lighting detectors)* | Siku 14 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| *vii.* | Maboya ya hali ya hewa (*Weather buoys)* | Siku 30 hadi 60 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **b.** | **Ulinganishaji vifaa vya hali ya hewa (comparison)** | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **c.** | **Uhakiki wa vifaa vya hali ya hewa (Calibration of meteorological instruments)** | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **d.** | **Uthibitishaji wa vifaa vya hali ya hewa (Verification)** | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **e.** | **Utoaji wa kibali (permit) cha kufanya shughuli za hali ya hewa** | Ndani ya mwezi mmoja baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **f.** | **Utoaji wa leseni ya usajili wa kituo cha hali ya hewa** | Ndani ya mwezi mmoja baada ya taratibu zote kukamilika |
| **Huduma** | | **Viwango** |
| **g.** | **Usimikaji (installation)** | |
| viii. | Kituo kinachojiendesha chenyewe (Automatic Weather Station-AWS) | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| ix. | Kituo kinachoendeshwa na mtu (Manned weather station) | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| x. | Kituo cha kupima mvua | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| *xi.* | *Rada (*Radar*)* | Siku 30 hadi 60 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| *xii.* | *Kituo cha uangazi cha anga la juu (Upper air station)* | Siku 30 hadi 60 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |

| | |
|---|---|
| *xiii. Vifaa vya utambuzi vya matukio ya radi (Lighting detectors)* | Siku 14 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| *xiv.* Maboya ya hali ya hewa (*Weather buoys*) | Siku 30 hadi 60 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **h. Ulinganishaji vifaa vya hali ya hewa (comparison)** | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **i. Uhakiki wa vifaa vya hali ya hewa (Calibration of meteorological instruments)** | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **j. Uthibitishaji wa vifaa vya hali ya hewa (Verification)** | Siku 1 hadi 7 baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **k. Utoaji wa kibali (permit) cha kufanya shughuli za hali ya hewa** | Ndani ya mwezi mmoja baada ya mteja kukamilisha taratibu zote |
| **l. Utoaji wa leseni ya usajili wa kituo cha hali ya hewa** | Ndani ya mwezi mmoja baada ya taratibu zote kukamilika |

3. **Uangazi wa hali ya hewa**

Tutapima na kufanya uchunguzi wa hali ya hewa kulingana na taratibu, kanuni na viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa kwa ajili ya huduma mbalimbali kama ifuatavyo; -

| Huduma | Viwango |
|---|---|
| i. Hali ya hewa kwa ajili ya mfumo wa mawasiliano wa kimataifa (Global Telecommunication System-GTS) | **Kila baada ya saa 3 kuanzia saa 9 usiku kila siku** |
| ii. Hali ya Hewa Kilimo | **Kila Saa 3 asubuhi na saa 9 alasiri kila siku** |
| iii. Usalama wa Usafiri wa Anga | **Kila baada ya nusu saa au saa moja kuanzia saa 9 usiku kila siku kulingana na ukubwa wa kituo** |
| iv. Usalama wa Shughuli za Kwenye Maji | **Kila baada ya saa moja kuanzia saa 9 usiku kila siku** |
| v. Hali ya Hewa Maji (Hydrometeorological), Klimatolojia (Climatological), Vituo vya Mvua (Rainfall Stations) | **Kila Saa 3 asubuhi kila siku** |

4. **Mafunzo**
    i. Tutatoa mafunzo ya hali ya hewa kulingana na viwango vinavyokubalika na NACTE na WMO kwa kiwango cha **cheti kwa mwaka mmoja** na **stashahada kwa miaka miwili**; na
    ii. Tutatoa mafunzo mahsusi kulingana na mahitaji ya mteja.

5. **Ushauri Elekezi**
    i. Tutatoa Ushauri Elekezi (Consultancy) **ndani ya siku tano (5)** za kazi baada ya kupokea maombi; na
    ii. Tutatoa huduma za Ushauri Elekezi kulingana na makubaliano na mteja.
6. **Malipo mbalimbali**
    i. Tutatoa malipo kwa mtoa huduma ndani **ya siku thelathini (30**) baada ya kukamilsha taratibu na kuwasilisha hati ya madai.
    ii. Tutatoa majibu ya tathmini ya zabuni ndani ya siku sabini (70) baada ya zabuni kufunguliwa.
    iii. Tutajibu malalamiko ya mzabuni ndani ya siku 7 saba za kazi baada ya kupokea

7. **Andiko na Jarida la kitafiti la Hali ya Hewa.**
    **i.** Tutatoa andiko la tathmini ya hali ya hewa ya nchi kwa mwaka **kila mwezi Machi.**
    **ii.** Tutatoa Jarida la machapisho ya tafiti za hali ya hewa **kila mwaka mwezi juni**

8. **Huduma nyinginezo**
    i. Tutoa huduma katika sehemu ya Mapokezi ndani ya **dakika tano (5)** baada ya mteja kuwasili
    ii. Tutapokea simu ndani ya **miito mitatu (3)** ya kwanza
    iii. Tutajibu maulizo ya vyombo vya habari na wadau wengine ndani ya **siku mbili (2**) za kazi
    **iv.** Tutakiri kupokea barua pepe, nukushi, barua, mitandao ya kijamii ndani ya **saa 24 za kazi**

**WAJIBU WA MAMLAKA KWA MTEJA**

1. Kutoa elimu, mafunzo na ushauri kwa mteja
2. Kutoa huduma bora za hali ya hewa kwa ufanisi katika muda uliokubalika
3. Kushirikiana na wateja katika mashauriano ya kuboresha huduma zetu
4. Kutoa taarifa sahihi na za kuaminika kwa lugha rahisi inayoeleweka kwa heshima na kauli nzuri.
5. Kutoa huduma kwa wateja bila ubaguzi wa aina yoyote

**HAKI NA WAJIBU WA MTEJA**

**<u>Haki za mteja</u>**

i. Kusikilizwa, kupata faragha na kuhifadhiwa siri zinazohusu huduma aliyopewa
ii. Kupata huduma na taarifa kwa wakati kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa
iii. Kutoa maoni, pongezi au malalamiko kuhusu huduma husika
iv. Kuhudumiwa kwa heshima
v. Kuona taarifa zinazomuhusu kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa

**Wajibu wa mteja**

i. Kuzingatia sheria, taratibu na kanuni kuhusiana na huduma husika;
ii. Kugharamia huduma anazopata kulingana na taratibu na viwango vilivyopo;
iii. Kuitikia wito wa kutoa taarifa au ufafanuzi;
iv. Kutoharibu miundo mbinu kwa ajili ya utoaji wa huduma
v. Kumheshimu mtoa huduma;
vi. Kutokuomba, kutokupokea wala kutoa rushwa
vii. Kutumia taarifa zinazotolewa na Mamlaka bila kuathiri usahihi wake
viii. Kutokusambaza huduma alizopewa bila idhini ya Mamlaka
ix. Kutunza kituo cha hali ya hewa kilichopo ndani ya umiliki wake kwa kuzingatia miongozo iliyopo.

**MREJESHO WA UTOAJI HUDUMA**

Mamlaka inakaribisha wateja na wadau wote kutoa mrejesho wa huduma inazozitoa. Tutapokea mrejesho wa aina yoyote kama vile maoni, mapendekezo, malalamiko, au ushauri kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu au Wakuu wa vituo kwa kutumia njia za mawasiliano ya, Barua **(mkono, posta), Sanduku la maoni, Barua pepe, Nukushi, Tovuti, Simu, Mitandao yetu ya kijamii, e-Mrejesho, au kufika moja kwa moja Ofisini kuonana na uongozi au mkuu wa mhusika.**

Mkataba huu ni nyaraka inayoishi, Mamlaka iitafanya mapitio kwa dhumuni la kuufanyia tathmini na kuboreshwa ili uweze kuendana na Matarajio ya Wateja. Mrejesho wa pongezi utatutia moyo katika kuendelea kuboresha zaidi huduma zetu.

**UTAMBULISHO WA MAMLAKA NA NJIA ZA MAWASILIANO;**

Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inapatikana Chuo Kikuu Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu.

Muda wa kazi ni **Saa 1:30 asubuhi hadi Saa 09:30 Alasiri**, Jumatatu hadi Ijumaa.

Mawasiliano ya ofisi ya Makao Makuu;

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
S.L.P 27,
1 Mtaa wa CIVE
**41218 Dodoma.**

Simu: +**255 22 2460706-8,**
Nukushi: +**255 22 2460735**
Barua pepe: **met@meteo.go.tz**
Tovuti: www.meteo.go.tz
Blog: **www.meteotz1950.blogspot.com**
Twitter: **www.twitter.com/tma_services**
Facebook**: @tmaservices**
Youtube: **@tanzaniametagency**
Instagram: **@tanzaniameteorological**
OnlineTV: **youtube.com/TMAonlineTV**

**Ofisi kuu za utabiri**

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania pia ina ofisi kuu zinazotoa tabiri na tahadhari za hali mbaya za hewa.

Mawasiliano katika ofisi hizi ni kama ifuatavyo;

| | | |
|---|---|---|
| 1 | **Ofisi ya Zanzibar** | Mkurugenzi Zanzibar,<br>Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,<br>S.L.P. 340,<br>10 Chukwani,<br>**Zanzibar 71214**<br>Simu: 0242230792<br>Nukushi: 0242231958<br>Barua pepe: znz@meteo.go.tz |
| 2 | **Kituo Kikuu cha Utabiri (CFO)** | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,<br>Ubungo Plaza, Ghorofa ya kumi,<br>388 Barabara ya Morogoro<br>S.L.P 3056,<br>**16102 Dar es Salaam**,<br>TANZANIA<br>Simu: 022 2460772<br>Nukushi: 022 2460772<br>Barua pepe: communication@meteo.go.tz |
| 3 | **Ofisi Kuu - Huduma za Hali ya Hewa Usafiri wa Anga** | Ofisi Kuu ya Uangazi<br>Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,<br>Barabara ya Nyerere, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA),<br>ACC/MET Complex,<br>S.L.P. 3056,<br>**Dar es Salaam,** Tanzania<br>Simu: 022 2460772<br>Nukushi: 022 2460772<br>Barua pepe: jnia@meteo.go.tz |

**Vituo Vikuu vya Hali ya Hewa**

Vituo vikuu vya hali ya hewa vinafanya kazi kati ya saa 12 hadi 24, Jumatatu hadi Jumapili. Vituo hivi ni kama vilivyoainishwa hapa chini;

| Na | Jina la Kituo | S.L.P | Na. ya Eneo | Namba ya Simu | Barua Pepe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 203 | 027 | 0736674360 | arusha@*meteo.go.tz* |
| 2 | Bukoba | 192 | 028 | 0762959909 | bukoba@meteo.go.tz |
| 3 | Dodoma | 27 | 026 | 0736674360 | dodoma@*meteo.go.tz* |
| 4 | Handeni | 115 | 027 | 0754650633 | handeni@*meteo.go.tz* |
| 5 | Iringa | 114 | 026 | 0754208845 | iringa@*meteo.go.tz* |
| 6 | Kigoma | 278 | 028 | 0737131906 | kigoma@*meteo.go.tz* |
| 7 | KIA | 3 | 027 | 0713339998 | kia@*meteo.go.tz* |
| 8 | Mahenge | 268 | 023 | 0738987638 | mahenge@*meteo.go.tz* |
| 9 | Songwe | 128 | 025 | 0765908951 | songwe@*meteo.go.tz* |
| 10 | Morogoro | 89 | 023 | 0738267155 | morogoro@*meteo.go.tz* |
| 11 | Moshi | 353 | 027 | 0733889535 | moshi@*meteo.go.tz* |
| 12 | Babati-Manyara | 356 | - | 0737185386 | babati@*meteo.go.tz* |
| 13 | Kilwa Masoko | 20 | 023 | 0737087279/ 0784822841 | kilwa.masoko@*meteo.go.tz* |
| 14 | Mtwara | 17 | 023 | 0737210057/ 0694944123 | mtwara@*meteo.go.tz* |
| 15 | Musoma | 89 | 028 | 0754361155 | musoma@*meteo.go.tz* |
| 16 | Mwanza | 701 | 028 | 0762605235 | mwz@*meteo.go.tz* |
| 17 | Same | 36 | 027 | 0737475027 | same@*meteo.go.tz* |
| 18 | Shinyanga | 248 | 028 | 0738225720 | shinyanga@*meteo.go.tz* |
| 19 | Singida | 563 | 026 | 0755215778 | singida@*meteo.go.tz* |
| 20 | Songea | 73 | 025 | 0735398364 | songea@*meteo.go.tz* |
| 21 | Sumbawanga | 306 | 025 | 0753577583 | sumbawanga@*meteo.go.tz* |
| 22 | Tabora | 40 | 026 | 0737285663 | tabora@*meteo.go.tz* |
| 23 | Tanga | 977 | 027 | 0734031910 | tanga@meteo.go.tz |
| 24 | Pemba | 169 | 024 | 0777461440 | pemba@meteo.go.tz |
| 25 | Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa Kigoma | 301 | 028 | 06520188 | nmtc@*meteo.go.tz* |

Vituo vya hali ya hewa kilimo vinafanya kazi kati ya saa 12 hadi 24, Jumatatu hadi Jumapili. Vituo hivi ni kama vilivyoainishwa hapa chini;

**VITUO VYA HALI YA HEWA – KILIMO**

| Na | Jina la Kituo | S.L.P | Na. ya Eneo | Namba ya Simu | Barua Pepe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Hombolo-Dodoma | 203 | 027 | 0769896071 | hombolo@*meteo.go.tz* |
| 2 | Igeri - Njombe | 299 | - | 0733339502/ 0754208845 | igeri@*meteo.go.tz* |
| 3 | Ilonga - Kilosa | 75 | - | 0717612286 | ilonga@*meteo.go.tz* |
| 4 | Kibaha - Pwani | 30460 | 023 | 0736438750/ 0764438750 | kibaha@meteo.go.tz |
| 5 | Kizimbani - Zanzibar | 30031 | 023 | 0773648485 | kizimbani@*meteo.go.tz* |
| 6 | Lyamungu - Moshi | 159 | - | 0765989826 | lyamungu@*meteo.go.tz* |
| 7 | Mlingano -Tanga | 3004 | - | 0734031910 | mlingano@*meteo.go.tz* |
| 8 | Naliendele - Mtwara | 89 | 023 | 0737210057/ 0694944123 | naliendele@*meteo.go.tz* |
| 9 | Tumbi -Tabora | 509 | 023 | 0737285663 | tumbi@*meteo.go.tz* |
| 10 | Ukiriguru -Mwanza | 306 | - | 0762605235 | ukiriguru@*meteo.go.tz* |
| 11 | Uyole -Mbeya | 1433 | - | 0755853588 | uyole@*meteo.go.tz* |
| 12 | Mbimba -Mbozi | 11 | | 0713630363 | mbimba.mbozi@*meteo.go.tz* |
| 13 | Matangatuani - Pemba | 169 | 024 | 0777461440 | matangatuani@*meteo.go.tz* |

Vituo vya hali ya hewa kwa ajili ya shughuli za kwenye maji vinafanya kazi kati ya saa 12 hadi 24, Jumatatu hadi Jumapili. Vituo hivi ni kama vilivyoainishwa hapa chini;

**VITUO VYA HALI YA HEWA SHUGHULI ZA KWENYE MAJI (MARINE)**

| Na | Jina la Kituo | S.L.P | Na. ya Eneo | Namba ya Simu | Barua Pepe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam Port Met | 3056 | 022 | 0737877374 | marine@*meteo.go.tz* |
| 2. | Kigoma Port Met | 278 | 028 | 0737131906 | kigoma.marine@meteo.go.tz |
| 3. | Itungi-Kyela Port Met | 344 | 025 | 0785667911 | kyela.marine@meteo.go.tz |
| 4. | Pemba Port Met | 169 | 024 | 0777461440 | pemba.marine@meteo.go.tz |
| 5. | Tanga Port Met | 977 | 027 | 0734031910 | tanga.marine@meteo.go.tz |
| 6. | Zanzibar Port Met | 340 | 024 | 0773648485 | zanzibar.marine@meteo.go.tz |
| 7. | Mwanza Port Met | 701 | 028 | 0762605235 | Mwanza.marine@meteo.go.tz |
| 8. | Karema Port Met | | | 0746855884 | |